**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

1. **Afisa Elimu (W)- 0763-220-846**
2. **Afisa Taaluma-(W)0785-699-171**

**Shule ya Sekondari Lindi Girls**

**S.L.P 1070**

**Tarehe 15/6/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LINDI GIRLS, HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI MKOA LINDI MWAKA 2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya *…………..*

   Shule ya Sekondari Lindi Girls iko umbali wa kilomita moja (2) kutoka barabara kuu ya Lindi - Dar es saam, Mtaa wa Kilangala kaskazini magharibi kutoka makao makuu ya Manispaa ya Lindi. Shule ipo umbali wa kilometa takribani **50** toka Lindi Mjini. Ili uweze kufika shuleni kwa urahisi kutokea Dar es salaam, panda mabasi yaendayo Lindi/Mtwara//Masasi/Tunduru/Nachingwea/Ruangwa shuka kijiji cha Kilangala (kabla hujafika Lindi mjini). Aidha kutoka stendi ya kijiji wa Kilangala hadi shuleni kuna umbali wa **KM 2.** Tumia usafiri bodaboda hadi shuleni kwa Tshs **1,000/=**

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/8/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/8/2023**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/8/2023**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-**

**2.1 Sare ya Shule**

i. Sare ya Shule hii ni sketi mbili za **Dark Blue**. Sketi ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi.Sketi ziwe na mkanda mpana (Belt), upana wa belt usizidi sentimeta 05 au inchi moja na nusu. Marinda mawili mbele yanayo tengeneza V, Sketi isibane iwe na upana wa kutosha.

ii. Shati (blauzi) nyeupe mbili (2) au za mikono mifupi tetroni
   (i) Viatu vyeusi (Visiwe na Kisigino Kirefu-high heels) jozi mbili (02) au zaidi
   (ii) Soksi nyeupe/Nyeusi jozi mbili (2) au zaidi.
   (iii) Kwa wanafunzi wa Kiislamu: Vazi la Msikitini. Suruali nyeusi ya heshima na isibane. Blauzi nyeusi ndefu ipite magoti na yenye mikono mirefu. Hijabu ya tetroni nyeupe/juba na sio mtandio, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi.
   (iv) Bukta nyeusi na Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.
   (v) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
   (vi) Sweta 2 za rangi ya Blue;
   (vii) Nguo za Kushindia (Shamba dress) rangi ya Blue Bahari
   (viii) T-shirt 1 ya rangi ya Blue

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Aje na godoro 01 la futi 3x6
ii. Shuka za Kulalia mbili za futi 3 x 6 rangi ya Pink.
iii. Taulo
iv. Vitabu kulingana na Tahasusi yake
v. Aje na kifaa kimoja kulingana na mkondo wake, kama ilivyobainishwa hapa chini:

   **PCB – Kwanja na Reki, CBG – Jembe, PGM - Panga**

vi. Soft broom moja na Hard broom 1,
vii. Mfagio wa kukaushia maji (drier),
viii. Fagio la chelewa moja (01), Brashi ngumu (1) ya kusugulia choo yenye mpini mfupi wa mbao/mti moja (01) kwa ajili ya kusafishia sinki la choo.
ix. Alete container lenye mfuniko/sahani, bakuli,kikombe na kijiko (vyombo vya chakula)

x. Daftari (Kaunta books) quire three zisizopungua kumi (10)
xi. Picha pasport size 4
xii. Ream moja ya karatasi A4 (photocopy paper) kila muhula, kwa mwaka ream 2.
xiii. Mathematical set moja (01) kwa matumizi yake awapo darasani.
xiv. Kwa wanafunzi watakaosoma ***BAM*** *au* ***ADVANCED MATHEMATICS*** ni vizuri wanunue Scientific Calculator.
xv. Graph pad moja (1) kwa mwaka
xvi. Alete chandarua/Net - futi 3 x 6 Nyeupe au Blue
xvii. Disecting kit ( kwa wanaosoma Biology).
xviii. Koti la maabara jeupe kwa wanafunzi wote

### 2.3 Michango Mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **Jumla** | | **80,000/=** |

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule (nywele ziwe fupi muda wote)
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

### 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**NB**. Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA.**

1. **AFISA ELIMU SEKONDARI 0713-346-015**
2. **AFISA ELIMU TAALUMA SEKONDARI 0785-699-171**

## FORM NO.1: MEDICAL EXAMINATION

## PRESIDENT'S OFFICE
## REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Lindi Girls Secondary School

P.O BOX 1070

LINDI.

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**.

Please examine Miss …………………………………………………………………… as her physical and Mental fitness for admission as a form …………………….. Students at Lindi Girls' Secondary School in the year ………………

Your sincerely.

HEADMISTRESS

The headmistress,

I have examined Miss ……………………………………………………… as shown and consider that she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time secondary school education.

1. Vision with/without glasses. Right ……………………… Left ………………………
2. Blood pressure …………………………… Hemoglobin ………………………
3. Hearing ………………………………………………………
4. Urine (a) Albumen………………………… (b) ...........................
5. a) Venereal diseases…………………(b) Bilharzia............................
6. Pregnancy ………………………………………………………
7. Neurosis………………………………………………………
8. Is there any abnormality of : (a) The heart…………………………….
   b) Lungs ……………………… c) The spleen …………………
9. Are there serious diseases. E.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes, etc. ………………………………………………………………………..

Date ……………… Signature of the medical Officer ………………

Station ………………… Designation ……………………

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI.**

1. (a) Jina la mwanafunzi …………………………………………………..
   (b) Anuani …………………………………..
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………..
3. Shule aliyomalizia darasa la saba …………………………
   Mwaka ……………………………………………
4. Mkoa anaotoka …………………………
   Wilaya alipozaliwa ……………………………..
5. Tarafa anayotoka ……………………….. Kata atokayo ……………………
6. Kijiji anachotoka ………………………….. Mtaa anaotoka ……………………
7. Jina la Mtendaji wa (a) Kata ………………………. (b) Mtaa/Kijiji ……………
8. Jina la (a) Balozi wa nyumba kumi ……………………….
   (b) Mwenyekiti wa Mtaa ……………………………
9. Michezo anayopendelea

| **Na.** | **Jina la Mchezo** |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |

11. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| **Na.** | **Aina ya Uongozi** | **Shule** | **Mwaka** |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo na sitapata chini ya alama 50 chini ya 100 kwa kila mtihani,zoezi au jaribio nitakalofanya hapa shuleni.

**Jina la Mwanafunzi …………………………………….. Sahihi ……………….**
**Tarehe …………**

**FOMU NAMBA 3.**

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ………………………………………………..
2. Kazi anayofanya mzazi ……………………………………………………..
3. Anuani ………………………………………………………………..
4. Namba ya simu …………………………………….
5. Mkoa ……………………..Wilaya …………………………… Tarafa …………
Kata ……………………………… Kijiji …………………….Mtaa ……………

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mwanafunzi atakuwa anakwenda wakati wa likizo

   Mahali ……………………………………. Kwa nani …………………………..

7. Majina ya viongozi/Wazazi /walezi atakakokuwa anakwenda wakati wa likizo
   Jina la Baba /mlezi/ndugu ………………………………………..
   Jina la mama/mlezi ………………………………………………….
   Mtendaji wa Kata …………………………… Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………
   Mwenyekiti wa Mtaa …………………………………………….
   Balozi wako wa nyumba kumi ……………………………………….

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………… ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Lindi Wasichana katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya. Ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule pale itakapobidi.

**Jina la Mzazi/Mlezi ……………….Sahihi ……..…… Tarehe …………….**

**FOMU NA.4**

**FOMU MAALUM YA TAARIFA ZA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

Ndugu wa karibu wa mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao.
Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo litatokea.

**(Ambatanisha passport size 4 za ndugu wa karibu)**

**1. (a)Jina ____________**
(b)Uhusiano: ______________________________
(c)Anwani:_________________________________________________
(d)Namba ya Simu:________________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: _______________________
Tarehe: ______________________________

**2 .(a)Jina**______________________________________________
(b) Uhusiano: __________________________________________
(c) Anwani:________________________________________________
(d) Namba ya Simu:______________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: _______________________
Tarehe: ______________________________

**3. (a)Jina**___________________________________________________
(b) Uhusiano: _______________________________
(c) Anwani:________________________________________________
(d) Namba ya Simu:_____________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: _______________________
Tarehe: ______________________________

**4. (a)Jina**___________________________________________________
(b) Uhusiano: _______________________________
(c) Anwani:________________________________________________
(d) Namba ya Simu:_____________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: _______________________
Tarehe: ______________________________